PRH inakupendekezea:

Kufuata warsha mbali mbali zinazotolewa katika siku 5 mfululizo, au katika vipindi vya mwisho wa wiki au vipindi kadhaa muda wa jioni.

Warsha zinatolewa kwa watu 15.

- PRH inatoa mafunzo ya kulea vikundi vya ukuaji kwa wale ambao baada ya kufuata warsha wanapenda kuielewa kwa kina.
- Inatoa pia ushauri kwa watu binafsi.
- Inawaelekeza wanawarsha wanaotaka kufuaata programu za kujilea wenyewe.

Mfumo wa mafunzo ya PRH ni wa taratibu, hatua kwa hatua.

- Washiriki wanafundishwa kuandika mag'amuzi ya nafsi zao na kushirikishana na wengine mang'amuzi yao ya maisha. Inatoa miongozo ya kujichanganua nafsi na pia miongozo ya kinadharia kuhusu zana za PRH za kumwezesha mtu kuendelea vyema katika maisha na kuwajibikia maendeleo yao.

Wakufunzi wa PRH Tanzania:

Sr. Rita Oscar,
Daughters of Mary Tabora
P.O. Box Singida
SINGIDA
Mobile 255784375091
Ritaoscar2002@yahoo.co.in

Sr. Archangela Massawe,
The Sisters of Our Lady of Kilimanjaro
S.L.P. 925
MOSHI
Mobile 255784640649
archangelamassawe@gmail.com

Sr. Catherine Ng'Wilwa
Daughters of Mary Tabora
P.O Box 396
KIPALALA- TABORA
Mobile 255 786 450 825
ncatherine2260@gmail.com

Sr. Magreth Lazaro Mahenge
Unitas for Africa
P.O. Box 1003
BIGWA – MOROGORO
Mobile 255 764 569 964
magrethlazaro@yahoo.com

Sr. Noella Naman
St. Catherine Monastery
P.O. Box 283
KARATU – ARUSHA
Mobile 255 686 240 225
Mobile sabrro45@gmail.com

Ni Wakufunzi wa PRH tu wanaotambuliwa na PRH kimataifa wanaoruhusiwa kutoa mafunzo ya PRH.

prh
Personality and Human Relations
TANZANIA



TAARIFA ZA PRH

WASHIRIKI

Watu wazima, au Vijana waliohamasika kuboresha ubora wa maisha yao





"Mipango ya elimu ya PRH ni kwanza na katika yote kazi ya kujigundua kuliko mafunzo ya kupokea tu."

"Tunapojigundua na kujifahamu tunatambua ndani mwetu nguvu ya maisha na njia mpya ya kuishi"

Andre' Rochais
Mwazilishi wa PRH

PRH
Utu na Mahusiano ya Kiutu
TANZANIA

PRH NI NINI?
Ni shule ya Kimataifa inayotoa mafunzo kwa vijana na watu wazima

UTUME WA PRH
Unashughulikia uuaji wa watu ambao vipaji vyao vitaifanya dunia iwe mahali pazuri zaidi pa kuishi.
Tunatoa mafunzo kwa watu binafsi, wanandoa,wataalamu mbali mbali ambao wana mtazamo na mwelekeo chanya kuhusu ukuaji wa mwanadamu na mahusiano yao.

Mafunzo hayo yanawasaidia watu kuzitafiti nafsi zao na kujifahamu wao ni nani.

DIRA YA PRH
- Tunaamini kuwa nafsini mwa kila mwanadamu kuna mang'amuzi yanayowafananisha ambayo yanapita mipaka ya mila na imani zao.

- Ndani ya nafsi ya kila mwanadamu kuna nguvu ya ukuaji inayomhimiza mtu kuishi na kutekeleza maweza yake.

- Kila mtu ana nafasi na majukumu ya kutekeleza katika jamii kama akisaidiwa kugundua na kutumia vipaji vyake.

- Ni mtazamo wetu kuwa watu wanaweza kufikia hatua ya kuishi kwa uhuru na usawa.

THAMANI ZA PRH

Wakufunzi na Marafiki wa PRH wanaishi thamani zifuatazo kumhusu mwanadamu;

- **Heshima** kwa mwanadamu, katika uwezo wake wa kuwa huru, kujitegemea,-kuthaminika na upekee wake ni kipaumbele chao.

- **Ufanisi** wa mwanadamu unajidhihirisha katika:
.Kukidhi inavyotakiwa malezi ya kumwezesha mtu kukuza thamani zake za kina na kuanza mwelekeo mpya wa maisha.

- **Mshikamano**.Wanakuza mshikamano na wanafunzi wao, kwa kuafikiana viwango vya malipo, ili mafunzo yao yaweze kutekelezeka na pia wamejenga ukaribu na watu wote bila kujali tofauti za kiitikadi.

- Wamejenga mfumo wa kuchangia mafunzo hayo ili kuwafikia wale ambao hali ya uchumi ni ngumu kwao.

Wana hamu kubwa ya kukuza utu. Wanafunzi wote wa PRH wanaishi ndani mwao hamu hii. Ni nguvu inayowahimiza kutoka ndani. Ni ya muhimu katika kuboresha maisha katika jamii.

ELIMU YA PRH ni mafunzo kwa ajili ya ukuaji na maendeleo ya mtu binafsi .

- Mafunzo yanamwelekeza mtu namna ya kugundua vipaji vyake vinavyomtambulisha jinsi alivyo, vinavyomsaidia kuishi ukweli wa nafsi yake na kukuza uwezo wake wa kuishi vizuri na watu wengine na kufikia furaha ya kina.

- Mafunzo yanatolewa na Wakufunzi na washauri wa PRH ambao wamehitimu na kupata shahada inayotolewa na PRH Kimataifa.

PRH inakualika:
- Kuitambua na kuishi nafsi yako ya ndani.
- Kugundua thamani zako za kina na nguvu yako kuendelea kukua.
- Kuendelea kugundua maelekeo na tendaji zinazokuzuia kuishi kikamilifu zaidi nafsi, kushindwa kushika nafasi yako kati ya wengine na kuhusiana nao vizuri.
- Kujifunza kusahihisha shida zako za tabia na tendaji zako za shida.
- Kufikia kuweza kuishi maisha yenye maana na yanayokuridhisha.